# *UPAMBANUZI WA ROHO*

Baba yetu wa Mbinguni, nataka kutamka, ikiwa ninaweza asubuhi hii jinsi ninavyojisikia moyoni mwangu kuhusu mmoja aliye Mtakatifu wa Watakatifu aliyeshuka kuja duniani kukomboa mwenye dhambi kama mimi na nina hakika ya kwamba wahudumu hawa walio hapa sasa, wanaweza kujisikia hivyo, ya kwamba ni kwa neema Yako ambapo tumefanywa wahudumu wa agano hili ambalo Wewe umeisha toa kwa jamaa ya Adamu iliyoanguka na tumekusanyika hapa Bwana si kwa kusudi lingine ila kujua na kujifunza tujue hasa mapenzi ya Mungu na kile kinatulazimu kufanya kumdhihirisha Kristo kwa watu wa kizazi hiki. Tukijua hakika ya kwamba katika siku ya hukumu tutakabiliana ana kwa ana na kizazi hiki. Na tukiwa wahudumu, tutakuwa mahakimu. Na watu tuliowazungumzia, na nia zao kuhusu Neno ambalo tunawaletea, zitaamua kikomo chao cha Milele. Kwa hivyo, Bwana, katika siku hiyo tungekuwa hakimu wa kukitetea au kukishtaki kizazi ambacho tumekihubiria.

2 Baba, Mungu, tafadhali, kwa Jina la Yesu, hebu na tusiseme neno moja ambalo lingekuwa kosa. Lakini tupate kuwa na mioyo minyenyekevu na nia zilizo safi ili tupate kupokea mambo yaliyo Yako, tupate kuwa na uwezo kuenda nje katika sehemu mbali mbali za kazi, baada ya leo, na—na tupate kujiandaa vizuri zaidi kwa ajili ya mkutano wetu pamoja nawe asubuhi hii. Tujalie, Bwana. Mbona usije uwe mnenaji wetu na masikio yetu, na ulimi wetu na mawazo yetu? Hebu kutafakari kwa moyo wangu, na mawazo ya nia yangu na chote kilicho ndani yangu, na ndani ya hawa ndugu zangu na dada zangu, na yakubalike machoni Pako, Bwana, ili kwamba tukaweze kujazwa na kuamrishwa na Roho Wako, wa Uwepo Wako hapa, hivi kwamba chumba hiki kingekuwa . . . chumba, si sana sana jengo ambamo tunaketi, bali jengo ambamo tunaishi ndani yake, lote liwe wingu la Utukufu wa Mungu. Tukaweze kutoka hapa asubuhi hii tukijaa sana Roho Mtakatifu hata tupate kuwa imara zaidi ya wakati wowote maishani kuupeleka Ujumbe kwa kizazi kinachokufa ambacho tunaishi ndani yake. Tusikie, Bwana, na ukanene nasi kwa Neno Lako, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Mwanao na Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Amina.

3 Nataka kusoma, asubuhi hii, se—sehemu ya Maandiko lipatikanalo katika Zaburi, Zaburi 105. Nataka kusoma tu sehemu. Ninyi ambao huyaandika Maandiko yanayosomwa, ninaona wengi wao na wakiwa walikuwa wahudumu na kadhalika. Ni vizuri kusoma Neno. (Na, sasa, kwa kawaida wao huondoka saa ngapi, karibu saa sita? Wasemaje? Asante.) Zaburi 105:

*Mshukuruni BWANA: liitieni jina lake, Wajulisheni watu matendo yake.*

*Mwimbieni, mwimbieni kwa Zaburi, Zitafakarini ajabu zake zote.*

*Jisifuni kwa jina lake takatifu, Na ufurahi moyo wao wamtafutao BWANA.*

*Mtakeni BWANA na nguvu zake, Utafuteni uso wake sikuzote.*

*Zikumbukeni ajabu zake alizozifanya, Miujiza yake na hukumu za kinywa chake.*

*Enyi wazao wa Ibrahimu, mtumishi wake; na Enyi wana wa Yakobo, wateule wake.*

*Yeye, BWANA, ndiye Mungu wetu; Duniani mwote mna hukumu zake.*

*Analikumbuka agano lake milele; Neno lile aliloliamuru vizazi elfu.*

*Agano alilofanya na Ibrahimu, Na uapo wake kwa Isaka.*

*Alilomthibitishia Yakobo liwe amri, Na Israeli liwe agano la milele.*

*Akisema, Nitakupa wewe nchi ya Kanaani, Iwe urithi wenu mliopimiwa.*

*Walipokuwa watu wawezao kuhesabiwa, Naam, watu wachache na wageni ndani yake,*

*Wakatanga-tanga toka taifa hata taifa, Toka ufalme mmoja hata kwa watu wengine.*

*Hakumwacha mtu awaonee, Hata wafalme aliwakemea kwa ajili yao.*

*Akisema, Msiwaguse masihi wangu, Wala msiwadhuru nabii zangu.*

4 Bwana na abariki usomaji wa Maneno Yake. Nina Maandiko machache yameandikwa hapa mahali fulani ambayo ningaliyarejea labda tunapoendelea.

5 Nashangaa, leo, ni nani atakayekuwa Rais wa pili? Mnajua, uchaguzi unaanza. Ni nani atakayekuwa Rais kipindi hiki? Vipi kama nilijua? Kuna mmoja tu ajuaye, na huyo ni Mungu. Vipi basi kama Mungu angalinifunulia ni nani atakayekuwa Rais wa pili, na ningesimama hapa Phoenix na kubashiri ya kwamba mtu fulani angekuwa Rais afuataye wa Marekani? Na wangaliweka hilo magazetini na kadhalika, na ningelilipata kikamilifu. Lingekuwa kamilifu, na iwe kwamba yote ambayo nimeisha sema yangetimia. Lakini ingefaa nini? Inafaa nini, kwa vyovyote, kama mimi—kama mimi ningetenda jambo kama hilo? Magazeti yangelitangaza hilo, na lingetoka nje pengine, ikiwa

mtu kama huyo angaliweza kufanya ubashiri wa namna hiyo na ukawa wa kweli, magazeti yote ya kila siku na ya mara kwa mara yange—yangetangaza ubashiri huo.

6 Lakini mnajua ya kwamba Mungu hafanyi mambo kama hayo. Mungu hatumii nguvu Zake na vipawa Vyake kwa upumbavu. Itakuwa, yeyote aliye Rais, atakuwa Rais. Na kujua sasa ni yupi angalikuwa Rais, haingetusaidia hata kidogo. Haingalitufanyia hata chembe moja ya wema kwetu kujua ni nani atakayekuwa Rais. Kwa hivyo, basi, Mungu hafanyi mambo haya namna hiyo.

7 Na, tena, ikiwa nilifanya ubashiri kama huo na unatimia, na magazeti ya kila siku yakauandika, na magazeti ya mara kwa mara, basi ingalikuwa kwa ajili ya utukufu *wangu*. Watu wangesema, "Tazameni jinsi Ndugu Branham alivyo nabii mkuu. Alituambia muda mrefu kabla haijatukia ni nani hasa atakayekuwa Rais." Na hiyo ingalikuwa kwa utukufu wangu. Lakini Mungu hataki . . . Yeye hapendezwi kufanya mambo kwa ajili ya utukufu wangu, au kwa—kwa utukufu wa mtu mwingine yeyote. Yeye hupendezwa na kutenda mambo kwa utukufu Wake, jambo litakalofaidi.

8 Kama alivyosema Paulo, "Ikiwa tunanena na lugha na hatuna mfasiri, itatufaidi nini? Tunajitukuza tu sisi wenyewe," na, hiyo ni, au "kujijenga sisi wenyewe." Hiyo ni kama haifai kwa Mungu. Mungu anataka kujengwa Mwenyewe. Nasi hatupaswi kujijenga wenyewe, bali kumjenga Mungu kwa yote tutendayo.

9 Kwa hivyo basi, naamini asubuhi hii, kama nilijua atakuwa nani na hasa ni lini angalichaguliwa, na, lo atashinda ama kushindwa kwa kura ngapi, au chochote kile, haingefaidi hata kidogo kuwaambia. Ingalikuwa heri kwangu kuwa kimya tu kama nilijua. Si kujaribu kuitangaza, kwa sababu pangekuwa—hapangekuwa na sababu kwangu kufanya hivyo. Kwa sababu, itakuwa hivyo, haidhuru, na haitufanyi tofauti sana ni nani atakayekuwa Rais.

10 Lakini, Mungu, anapotumia karama Zake, Yeye huzitumia kwa ajili ya utukufu Wake Mwenyewe, na kwa utukufu wa watu Wake, kwa ajili ya utukufu wa Kanisa Lake, kwa kuujenga Mwili wa Kristo, na kwa ajili ya utukufu wa Ufalme wa Mungu. Hiyo ndiyo sababu Yake ya kutoa mambo haya katika Kanisa Lake, sababu Yake, ya kuwa na waalimu, nabii, wainjilisti, wachungaji. Wao wako kwa ajili ya kulijenga Kanisa na kwa utukufu wa Mungu. Nabii hapaswi kutoka na kuchanganyikana na ulimwengu na kujaribu kupokea zawadi kama alivyofanya Balaamu, na kusababisha upotovu mwingi au—au kupata fedha kwa hilo au kitu fulani. Kama ni nabii, anapaswa kumfunua Mungu kwa Kanisa na kukaa nje ya mambo ya ulimwengu. Yote ni kwa utukufu wa Mungu!

11 Sasa sisi tuna . . . na ninadhani ni jambo njema kwetu, kama wahudumu, kufuata utaratibu wetu, tuonapo mambo kama hayo ulimwenguni kama tuyaonayo leo. Na tuna utaratibu kutoka kwa Mungu, nao ni wa kupambanua roho, kujaribu roho. Ninaamini ya kwamba hilo ni somo kubwa sana kwa kanisa leo, ni kujaribu roho ya kila kitu, kuwa na upambanuzi wa roho. Mimi sidhani ya kwamba tunapaswa kamwe, kwa vyovyote, kujaribu kamwe kumhukumu mtu kwa dhehebu lao, au kwa kundi wanalokusanyika nalo, hata wawe Wamethodisti, Wapresbateri, Wapentekoste, au—au chochote kile. Hatupaswi kamwe kumhukumu mtu kwa dhehebu lake. Tunapaswa daima kumhukumu yeye kwa roho aliye naye, mnaona, roho. Kwamba ni wa mvua ya vuli au mvua ya masika au ya ndani, mvua ya nje au bila mvua au chochote kile, hatupaswi kamwe kumhukumu yeye kwa hayo, bali, kwa roho yake. Inatupasa kupambanua roho. Chunguza kile kilicho niani mwa mtu, alicho nacho . . . anachojaribu kupata. Kama huyo mtu, kwa karama, haidhuru karama hiyo ni kubwa jinsi gani . . .

12 Sasa ninataka kuliambia Kanisa jambo hili asubuhi hii, ambalo, katika madhehebu mbali mbali mngali bado Kanisa la Mungu aishiye, pamoja. Na hili ndilo jambo ninalotaka kuleta kwenu, mwaona, ya kwamba sisi kwa kweli hatutenganishwi. Sisi tu mawe ambayo yamekatwa katika umbo mbali mbali, sote kwa utukufu wa Mungu.

13 Sasa, kuna mengi sana katika siku tunayoishi, kuhusu "karama." Watu wengi mno huhukumu watu kwa karama walizo nazo. Vema, ninaamini mambo haya ni karama. Ninaamini ya kwamba yale tunayoona yakitendeka ni karama, na ni karama ambazo zimetolewa na Mungu. Lakini, sisi, ikiwa sisi hatuzitumii katika njia iliyo sahihi ambayo Mungu alikusudia zitumiwe, basi tungefanya udhuru zaidi kwa karama hizo kuliko vile tungefanya kama hatungekuwa na karama. Majuzi usiku nilitoa matamshi mimbarani, nikisema hili, kwamba afadhali nione upendo wa kindugu ukidumu katika kanisa, kama tusingalikuwa na kisa kimoja cha uponyaji au kitu kingine chochote. Mnaona, ni lazima tujue mambo haya yako kwa ajili gani.

14 Sasa, mtu akija na ana karama kubwa, haidhuru ikiwa ni wa dhehebu letu au dhehebu lingine, msimhukumu yeye kwa dhehebu alimotoka, jinsi anavyovalia, lakini kile unachotaka kuona ni yale anayojaribu kufanya kwa hiyo karama. Ana kusudi gani. Ikiwa anajaribu kutwaa ushawishi wake na kujijengea mwenyewe jina kuu toka kwake, nitakuwa na upambanuzi wa kiroho wa kutosha kujua hilo ni kosa. Haidhuru yeye ni mwalimu mkuu jinsi gani, jinsi alivyo na nguvu, jinsi alivyo mwenye akili, au karama yake inavyotenda kazi, ikiwa hajaribu kufanikisha jambo fulani kwa faida ya Mwili wa Kristo, upambanuzi wako wa kiroho ungekwambia ya kwamba

hilo ni kosa. Haidhuru jinsi ilivyo sahihi, jinsi ilivyo kamilifu, jinsi ilivyo, ni makosa ikiwa haitumiwi kwa ajili ya Mwili wa Yesu Kristo.

15 Kupata kitu, huenda ikawa ana karama kuu ambayo anaweza kuwavutia watu pamoja kwa akili kuu au kwa nguvu za kiroho, ambazo kwazo angeweza kuwavuta watu pamoja, na huenda ikawa anajaribu kutwaa karama hiyo na kujifanya mwenyewe mashuhuri, ili kwamba atakuwa na jina kubwa, hivi kwamba ndugu wale wengine watamtazama yeye kama mtu fulani mkubwa. Basi hilo ni kosa. Huenda ikawa yeye anajaribu ku—kujenga jambo fulani hapa ambapo anataka kila mtu aondoke kwenye picha na kumwachilia yeye na kundi lake wawe ndio picha. Hilo bado ni kosa, mwaona.

16 Lakini iwapo ana karama ya Mungu naye anajaribu kuujenga Mwili wa Kristo, basi sijali anatokana na nini. Wewe humpambanui huyo mtu, unapambanua roho, uhai ulio ndani ya huyo mtu. Na hivyo ndivyo Mungu alituambia tufanye. Hata mara moja hatukuagizwa kupambanua ku—kundi la huyo mtu. Lakini tulilazimishwa na kuamriwa na Mungu kupambanua roho iliyo ndani ya huyo mtu, yale anayojaribu kufanya, ni wapi roho aliye ndani ya maisha yake anakojaribu kumwongoza. Na basi, ikiwa tunaweza kuona kwamba anajaribu kuwaongoza watu (si kuwatenganisha bali kuwaunganisha) na kuleta Kanisa la Mungu aishiye, sio wote katika dhehebu moja, bali kwa kuelewana, ushirika, umoja wa roho. Basi ikiwa yeye ni mvua ya masika au vuli, au chochote kile, roho yake na kusudi lake ni sawa. Na roho iliyo ndani yake, haidhuru anatokana na kundi gani, Roho aliye ndani yake, anajaribu kuwaelekeza watu Kalvari, mbali naye mwenyewe au mbali na kitu kingine chochote, lakini analotaka kupata pekee in kuwaelekeza wao Kalvari. Hajali kwamba yeye anajulikana au la. Hajali kwamba dhehebu lake. . . ambalo ni sawa, mwaona, ni zuri, kama ni Mmethodisti, au Mpresbeteri, au Mkatoliki wa Kirumi, au chochote anachotaka kuwa kwa dhehebu.

17 Lakini anajaribu kufanya nini, kusudi la moyo wake analojaribu kupata? Ndipo unaweza kuona kilicho maishani mwa mtu huyu, kwamba madhumuni yake ni kwa ajili ya—ya dhehebu lake, kwamba ni kwa ajili yake mwenyewe, kwamba ni kwa ajili ya mambo ya ulimwengu, kwamba ni kwa ajili ya majina makubwa, kusema, "Nilibashiri, *hilo*, likaja kutimia sawasawa." Sasa, mnaona, hilo ni kosa papo hapo, kwanza. Lakini ikiwa yeye anajaribu kutumia kile Mungu alimpa, kama mwalimu, kama nabii, kama mwonaji . . .

18 Nabii wa Agano Jipya ni mhubiri. Sote tunajua hayo. Mhudumu awaye yote aliye mhubiri ni nabii, nabii wa Agano Jipya, ikiwa yu atabiri, kuhubiri, si kwa kujaribu kujijenga mwenyewe kujifanyia jina kubwa, au kujenga dhehebu lake. Ambapo anapaswa kuwa na dhehebu. Niko hapa bila hata moja,

lakini bado nahubiri yakupasa uwe nalo. Hiyo ni kweli. Kila mtu yampasa awe na kanisa la nyumbani. Yakupasa uwe na mahali, sio tu kuelea kutoka nguzo moja hadi nyingine, bali uwe na mahali ambapo unaenda kanisani na unapaita kanisa lako, mahali unapolipa zaka zako, na mahali ambapo unasaidia Mwendeleo. Jichagulie mwenyewe, lakini basi usimtenge kamwe ushirikani mtu mwingine kwa sababu yeye si wa kundi lako. Unaona? Pambanua roho yako na uone kama yeye ana kusudi lile lile moyoni, ndiposa mna ushirika moja kwa mwengine. Mnafanya kazi kwa Kusudi moja kuu. Hilo ni kusudi la Kristo. Nadhani ya kwamba hiyo ni kweli kabisa.

19 Sasa, kama tukiangalia kusudi na madhumuni ya manabii wa Agano la Kale, watu hao walikuwa na shabaha moja, na hiyo ilikuwa Yesu Kristo. Walikuwa na jambo moja ambalo kiini chao kwa jumla cha Agano la Kale kilijengwa, kule kuja kwa Masihi. Wao—wao hawakutoka na kufanya mambo kwa ajili ya pesa tu au kwa ajili ya sifa. Walikuwa na jambo moja, walikuwa na upako wa Roho wa Mungu, nao walibashiri kuja kwa Masihi. Na watu hao walikuwa na upako sana wa Roho, hata mara kwa mara wao walitenda kama Roho aliyekuwa ndani yao, yaonekana kama kwamba walinena habari zao wenyewe. Chunguza jinsi Roho wa Mungu alivyowafanya hao watu kutenda.

20 Tutachukua, kwa mfano, Musa, yule nabii mkuu, jinsi huyo mtu hakuwa na shabaha ya kujinufaisha binafsi hata kidogo. Angaliweza kuwa mfalme wa Misri. Angaliweza kuuweka ulimwengu chini ya miguu yake. Lakini kwa sababu alikuwa nabii moyoni, alikataa kuitwa mwana wa binti Farao, akiona ni afadhali kupata mateso na majaribu ya Kristo, akihesabu hazina za Mbinguni kuwa kuu kuliko hazina hizo za Misri. Alizisahau na kujinyima mwenyewe sifa za kilimwengu, anasa na yale—yale mambo yanayotolewa na maisha. Ilimbidi kutazama ng'ambo ya hayo. Mnaona, yeye—yeye angalikuwa hivyo.

21 Chukua tu mhudumu siku hizi, ikiwa ana ubatizo wa Roho Mtakatifu, na anajua ya kwamba kama akihubiri hilo neno, litapunguza sifa zake, litamweka kwenye maskini kikanisa kidogo mahali fulani, au labda nje barabarani. Lakini anajua ya kwamba kitu fulani kinawaka moyoni mwake. Yuaona Kuja kwa Bwana. Yeye hajali kwamba ana kanisa kubwa au kanisa dogo. Yeye hajali kwamba ana chakula cha leo au hana chakula. Yeye hajali kwamba ana mavazi mazuri au hana mavazi mazuri. Anajali tu kitu kimoja, na hicho ni Uzima ule ulio ndani yake ukipasa sauti. Yeye anajaribu kufanikisha jambo fulani kwa utukufu wa Mungu, na mtu huyo, katika kufanya hivyo, atatenda kama Uzima ule wa Roho aliye ndani yake. Mnanifuata? Yeye atatenda hivyo.

22 Mtazameni Musa alipofikia wakati ambao alionyesha, maisha yake yote yalikuwa Roho wa Kristo, kwa kuwa Kristo alikuwa ndani yake. Kristo alikuwa ndani ya Musa, kwa kipimo.

Sasa, ikiwa tunatambua, alizaliwa wakati wa mateso. Watoto waliuawa kujaribu kumpata, kama tu walivyomfanyia Yesu. Na tunatambua ya kwamba alipofikia mahali ambapo wana wa Israeli waliasi sana hata Mungu akachukizwa nao, naye akamwambia Musa, "Simama kando nami nitaliangamiza kundi lao lote, na nitakutwaa wewe na kuinua kizazi kingine."

23 Musa alijitupa mwenyewe njiani mwa hukumu ya Mungu, na kusema, "Nitwae mimi kabla hujawatwaa wao." Kwa maneno mengine, "Kabla hujawafikia wao, itakubidi Wewe upitie juu yangu."

24 Hivyo ndivyo hasa alivyofanya Yesu Kristo. Wakati Mungu angaliufagia uso wote wa dunia pamoja na hawa wenye dhambi, mimi na wewe, lakini Kristo alijitupa mwenyewe njiani. Mungu hangaliweza kufanya hivyo, Yeye hangaliweza kupitia juu ya Mwanawe.

25 Na Mungu alipoona Roho huyo katika Musa, akining'inia hukumuni pale kama msalaba, "Huwezi kuja kwao, itakubidi unitwae mimi kwanza," mnaona Roho ya Mungu ndani ya Musa? Na huku angalikuwa mfalme wa Misri, na huku angalipata kila namna ya anasa duniani, kupendwa na watu, na angalikuwa mfalme wa ulimwengu wakati huo. Lakini alichagua kuteswa na kupigwa, kwa kuwa alihesabu kudhulumiwa kwa Kristo hazina kubwa kuliko za Misiri. Mnaona, alijitupa mwenyewe njiani. Kwa nini? Ni Mungu ndani ya Musa aliyefanya hayo. Mtu wa kufikiria, wa kawaida, mwenye akili, hangefanya kamwe hivyo, angechukua njia iliyo rahisi. Kwa hivyo haidhuru jinsi Musa alivyoonekana kuwa mshupavu wa dini, alikuwa anajaribu . . . Mnaona, alikuwa wa kweli nabii wa Mungu, kwa maana anajaribu kufanikisha kitu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

26 Sasa, akiwa na karama yake kuu ya unabii yeye angalikuwa mtu mwenye hekima, angalisimama Misri na kusema, "Sasa ngojeni, nitatabiri jambo fulani. Nitasema jambo fulani," na kama ulivyo utabiri wake. Lakini ni . . . na, lo, angekuwa mwenye sifa duniani. Bali hilo halikuwa moyoni mwake. Halingekuwa moyoni mwake.

27 Kwa hivyo umwonapo mtu aliye na karama kuu, akijaribu kufanya kitu kujitukuza mwenyewe, upambanuzi wako wa roho hukwambia hilo ni kosa. Lakini Musa alikuwa anajaribu kupata kitu kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Haidhuru kilikuwa kibaya jinsi gani—kilionekana kiovu jinsi gani, jinsi kulinenwa, Roho ya Musa ilimwongoza yeye moja kwa moja kwenye wajibu wake. Roho iliyokuwa ndani yake.

28 Mtazameni Yusufu, Yusufu alikuwa . . . alipozaliwa, alipendwa na babaye na kuchukiwa na nduguze, mfano mkamilifu wa Kristo. Na jambo pekee . . . yeye alikuwa ndugu wa damu kwao, baba mmoja. Lakini sababu ya nduguze kumchukia,

bila udhuru, ni kwa sababu Mungu alimfanya nabii, wa kiroho, mwonaji. Na wao walimchukia kwa kusudi hilo. Lakini Yusufu hangeweza kujizuia, kwa maana Mungu alimfanya hivyo.

29 Basi chunguzeni Roho ya Mungu katika Yusufu. Chunguzeni aliyotenda. Hata yeye aliigiza sehemu ya Kristo. Yeye alichukiwa na nduguze, kapendwa na babaye, kwa sababu Roho alileta tofauti. Yeye alikuwa mtu wa kiroho. Aliona maono, alitafsiri ndoto. Yeye hakufanya hivyo kwa utukufu wake mwenyewe. Alifanya hivyo kwa sababu kulikuwa na kitu ndani yake, Roho ya Mungu. Yeye hangalikwenda nje kule yeye mwenyewe, na awe ametupwa shimoni, na kumfanya maskini mzee babaye kuhuzunika miaka hiyo yote, akauzwa kiasi cha karibu vipande thelathini vya fedha; katolewa shimoni, na akawa makamu wa Farao, mfalme wa ulimwengu wakati huo. Na katika chumba chake gerezani walikuwako mnyweshaji na mwokaji, na mmoja aliangamia na yule mwingine aliokolewa, kwa ubashiri wake, chumbani gerezani.

30 Je, mlitambua Yesu alipokuja, alipendwa na Babaye. Na babaye Yusufu alimpa joho lenye rangi nyingi (upinde wa mvua, agano). Na Baba, Mungu, alimpa Mwanawe, Yesu, agano, kisha nduguye Myahudi alimchukia Yeye bila sababu. Hakuwa na sababu ya kumchukia Yeye, Yeye alikuwa wa kiroho, na Yeye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa. Yeye alikuja kuyafanya mapenzi ya Baba, Yeye alikuja kutimiza Maandiko. Yeye alikuja kuwaletea amani, bali walikosa kumfahamu Yeye, na wakamchukia bila udhuru. Wao kwanza hawakujaribu kuona yale aliyokuwa akijaribu kufikiliza. Walimhukumu kwa sababu Yeye hakukubaliana nao. Walifanya . . . “Hujifanya Yeye Mwenyewe ni *fulani*. Hujifanya Mwenyewe kuwa Mungu.” Yeye alikuwa Mungu. Mungu alikuwa ndani Yake. Biblia ilisema Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akijionyesha Mwenyewe kwa ulimwengu. Yeye alikuwa Mungu wa Utukufu akionyesha utukufu wa Mungu.

31 Mtazameni Musa, hangejizuia kujitupa mwenyewe pale. Hakufanya hivyo kinafiki. Alifanya hivyo kwa sababu Mungu alikuwa ndani yake. Hata Yusufu hangaliweza kujizuia kuwa alichokuwa, kwa sababu ilikuwa Mungu ndani yake akifanya, au akijionyesha Mwenyewe dhahiri kupitia huyo mtu. Hakufanya hivyo kamwe kwa ajili ya utukufu wa kibinafsi.

32 Mtu yeyote yule . . . Laiti hao makuhani wangekuwa tu na upambanuzi wa roho, kama ninavyowazungumzieni asubuhi hii. Bila kujali jinsi ulimwengu ulivyonena juu yake, hata hivyo wao wangaliiisha jua kama wangaliangalia Neno, ikiwa wangaliona kusudi Lake. Yeye alikuwa daima akifanya hivyo kumtukuza Baba. Yeye alisema . . . Wao walisema, “Lo, mtu huyu ni mponyaji mkuu, Yeye hufanya mambo haya hivyo.”

33 Yeye alisema, "Siwezi kufanya kitu ila Baba anionyeshe Mimi. Si Mimi nizifanyazo kazi. Ni Baba akaaye ndani Yangu, Yeye hufanya kazi." Yeye hakujitwalia utukufu.

34 Wala mtumishi yeyote wa Mungu hangetwaa utukufu. Wala mtumishi yeyote wa Mungu hangetwaa karama ya Mungu na kujaribu kujitukuza mwenyewe, au kitu kinginecho, bali tendo lake la haki ni kufanya kitu kwa utukufu wa Mungu. Hiyo ndiyo sababu mnaona jambo lile lile leo. Ni lazima tuwe na upambanuzi wa roho, tukaone wanachojaribu kufanya watu. Wao wanajaribu kumtukuza Mungu? Wao wanajaribu kujitukuza wenyewe?

35 Sasa Roho wa Mungu akifanya kazi ndani ya mtu humfanya atende kama Mungu. Si ajabu Yesu alisema "Si imeandikwa, 'Ninyi ni miungu'? Na ikiwa waliwaita miungu ambao walijiliwa na Roho wa Mungu, mwawezaje kunihukumu Mimi, basi, nikiwa Mwana wa Mungu." Kama mngaliweza kuona Roho wa Mungu ndani ya Musa, ambaye, alikuwa Mungu. Musa alikuwa mungu. Yusufu alikuwa mungu. Manabii walikuwa miungu. Biblia ilisema walikuwa hivyo. Walikuwa miungu kwa maana ili . . . wao waliisha jisalimisha wenyewe kabisa kwa Roho wa Mungu, kwamba wao walikuwa wakifanya kazi kwa utukufu wa Mungu.

36 Na mtu anapokuwa na upako sana wa Roho . . . Sasa hebuni hili liingie kwenye kilindi chini ya ubavu wa tano upande wa kushoto. Mtu anapotiwa upako wa Roho wa Mungu, tabia zake, matendo yake, na kila kitu, ni Mungu akienenda ndani yake. Mara kwa mara anahukumiwa makosa.

37 Mwangalieni Daudi, katika Zaburi 23, yeye alilia, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" kama kwamba ilikuwa yeye, kama kwamba Daudi alikuwa mtu huyo. "Wote wapitiao karibu nami, hunifyonya kwa midomo yao."

38 Alikuwa na upako sana wa Mungu, alikuwa amejisalimisha kikamilifu sana kwa Mungu, na upako ulikuwa juu yake kwa wingi sana na alipolia kwa Roho wa Mungu, kama mtu fulani angalikuwa amesimama pale, angesema, "Naam, tazameni, yeye anadhani mtu fulani anamfyonya kwa midomo yake. Mbona Mungu amemsahau?"

39 Haikuwa Daudi, ilikuwa Roho akilia kupitia kwa Daudi. "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Mifupa yangu yote inanikondolea macho. Wamenizua mikono na miguu yangu."

40 Vema, mtu fulani alisema, "Msikizeni huyo mnafiki juu kule. Mikono ya nani iliyozuliwa?" Miguu ya nani iliyozuliwa? Huyo ni mwenye akili.

41 Lakini yule aliyekuwa na upambanuzi wa roho alijua ya kwamba huyo alikuwa Roho wa Mungu ndani yake akilia. Mtu awapo na upako wa Roho wa Mungu, yeye ana kitendo cha Mungu, na kitendo cha Mungu si cha kututenganisha kamwe.

Kitendo cha Mungu ni cha kutukusanya pamoja kwa kuwa tu mmoja katika Kristo Yesu, na kusudi la Mungu ni kutukusanya pamoja. "Pendaneni mmoja kwa mwingine."

42 Sasa, hao manabii wakuu, tunaona Roho akienenda kati yao, Yesu aliwaita wao "miungu." Yeye alisema walikuwa miungu. Sasa Roho alipowajilia wao kwa kipimo, bali alipokuja kwa yule Mmoja, Yesu, aliyekuwa Mwana wa Mungu, alimjilia Yeye bila kipimo, ukamilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake, kwa kuwa alikuwa mfano mkamilifu. Yeye alikuwa Mungu wa Utukufu akionyesha utukufu wa Mungu kwa watu, Mungu ndani yake akitembea-tembea. Chunguza maisha Yake, Agano la Kale lote, Yeye alikuwa kiini cha Agano la Kale. Manabii wote wa kale nyuma huko katika Agano la Kale walipasa sauti, si kwa ajili yao wenyewe, walipasa sauti chini ya Roho wa Mungu, akiwafanya wao watende kama Mungu kiasi cha kuwa waliitwa miungu, kisha ukamilifu wote wa Roho huyo ulidhihirishwa katika Yesu Kristo.

43 Mtazameni Daudi alipoondolewa kwenye kiti cha enzi kama mfalme wa Israeli, alikataliwa na watu wake, akikwea Mlima wa Mizeituni, kaskazini mwa Yerusalemu, naye akatazama nyuma juu ya mji na kulia kwa sababu alikuwa amekataliwa. Ilikuwa nini? Ilikuwa Roho wa Kristo.

44 Miaka mia tano baadaye, Mwana wa Daudi, Yesu, aliketi kwenye mlima ule ule, akiutazama ule mji, kama mfalme aliyekataliwa, akalia, "Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi ningalikukusanya wewe, (madhehebu yako mbali mbali na kila kitu) kama kuku anavyowakusanya makinda wake, bali hungetaka. Ningalifanya hivyo mara ngapi!"

45 Sasa Roho yule yule aliyekuwa ndani ya Daudi, ambaye alidhihirishwa kikamilifu katika Kristo, yu ndani ya Kanisa leo akiwalilia watu, "Ni mara ngapi ningaliwakusanya ninyi!" Na uonapo matengano na—na tofauti na—na undugu ukivunjika, na maisha ya Kikristo, mmoja dhidi ya mwingine, basi humfanya Roho wa Mungu aliye moyoni mwako alie. Unajaribu kupata kitu, nabii wa kweli wa Mungu, mwalimu wa kweli anajaribu kulileta Kanisa katika umoja wa roho, umoja wa roho, ili kwamba waweze kumtambua Mungu; wakijaribu kupata hilo haidhuru wametoka katika dhehebu lipi au chochote kile. Tuna upambanuzi wa roho kupambanua roho aliye ndani ya mtu, kuona kama ni Roho wa Mungu au la.

46 Sasa, tunaona Yeye alipokuwa hapa duniani, jinsi alivyoenenda akifanya mema. Ninaona jambo lingine linalonijia niani mwangu. Mliona Daudi alipokataliwa kama mfalme? Alienda nje ya mji, na maskini mmoja Mbenyamini, Mbenyamini, aliyedhaniwa kuwa ndugu yake, alipaswa kumsikitikia kwa sababu alikataliwa, lakini nini. . . Alikuwa kiwete. Na alijikokota pale na hali yake ya ulemavu, akimtupia

Daudi uchafu, na kumwita kila namna ya majina mabaya, na kumlaani katika Jina la Bwana, akimlaani Mfalme Daudi katika Jina la Bwana, huyu maskini mzee kiwete Mbenyamini.

47 Angalieni Roho wa Mungu na roho wa Ibilisi wakitenda kazi. Sasa, mkichunguza, alikuwa kiwete. Inawakilisha ulemavu wa kiroho wa watu leo ambao wanamfanyia dhihaka Roho wa kweli wa Mungu katika Kristo anayejidhihirisha Mwenyewe. Huyo alikuwa Roho wa Kristo katika Daudi akikataliwa kama mfalme. Na, leo, watu wanapowadhihaki watu ambao wamempokea Roho Mtakatifu na wanajaribu kufikiliza jambo fulani, kuwavuta Wamethodisti na Wapentekoste, na Wabatisti na Wapentekoste, na Wapresbeteri na wote, pamoja katika umoja, kama Mwili wa Kristo, na wao wanamwona Roho akitenda kazi, kasema, "Vema, tazama, huyo ni Mpentekoste. Mwondoshe! Ninamjua mmoja aliyemtorosha mke wa mtu mwingine. Ninamjua huyu aliyelewa. Namjua huyu aliyefanya *hili*. Ninajua huyu mmoja alifanya *hilo*." Yote haya, lakini wao ni wakubwa vya kutosha kuficha mambo yao, wanaweza kuficha. Bali Daudi aliwekwa wazi. Kwa nini? Alikuwa na Roho wa Kristo ndani yake.

48 Huyo mlinzi alisema, "Nikikate kichwa cha mbwa yule ambaye anathubutu kumlaani mfalme wangu?"

49 Angalieni Roho wa Kristo katika Daudi, "Mwachilie, kwa kuwa Bwana amemwambia anilaani mimi." Mnashika hilo? "Mwachilie, Bwana amemwambia anilaani mimi."

50 Badala yake, leo, tunataka kuinua ngumi zetu na kupigana naye, mwaona, kukata kichwa chake, "Ndio, mwondoeni, si wa kwetu"

51 "Mwachilie, Bwana amemwambia anilaani mimi." Huyo maskini kiwete akikimbia-kimbia pale, akimtupia uchafu Daudi.

52 Hivyo ndivyo wafanyavyo leo juu ya Roho wa Kristo. "Wao ni kundi la watakatifu wafingirikao. Wao ni—wao ni kundi la *hili*. Hamna chochote kwao. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna kitu kama Malaika. Hamna kitu kama manabii." Mambo hayo yote, "Siku za miujiza zimepita," wakitupa uchafu. Lakini waachilieni. Bali Daudi aliporudishiwa utawala, haleluya, aliporudi kama mfalme kamili wa Israeli . . . Msifadhaike, Yesu huyu, ambaye ndiye Roho tuliye naye leo, alitenda sehemu Yake, atarudi tena katika mwili wa nyama, mara ya pili, katika utukufu, mwenye nguvu na enzi.

53 Yule maskini mwenye kumtupia uchafu alianguka kifudifudi na kulalama. "Mwachilie," Roho wa Kristo ndani yetu. Msimwondoe ushirikani. Hebu tukumbuke ya kwamba mambo haya yote hayana budi kutimia. Tuna jambo moja la kutenda, tuendelee mbele. Mungu aliahidi ya kwamba Yeye angefanya kila kitu kitende kazi pamoja kwa wema kwa wao wampendaye.

Hebu tudumishe upambanuzi wa roho, tuweke shabaha yetu sahihi. Tuko hapa kumtumikia Mungu kila mmoja akishiriki, tukiendelea na kumtumikia Mungu. Ikiwa mtu ana aina baya ya shabaha, basi itakuwaje? Mnaona?

54 Sasa, tunagundua ya kwamba Roho wa Mungu alikuwa ndani Yake. Manabii wote wa kale walinena juu Yake. Roho yote, kwa sehemu, kila sehemu dogo, haikuwa ikijitukuza yenyewe (manabii wa kweli,) manabii wote wa kweli walikuwa wakimdhihirisha Yeye, wakinena juu Yake. Na kila kitu walichosema kilitimizwa ndani Yake. Ilionyesha alikuwa Roho wa Mungu ndani yao, kilitimizwa. Ilikuwa nini? Mungu akinena juu Yake. Mwaona? Mungu akijidhihirisha Mwenyewe kupitia kwa hawa manabii.

55 Bila kutwaa utukufu, "Ni nani atakayekuwa Rais wa pili? Na ni nani atakayekuwa *hiki*?" Na kukugonga kichwani, "Tuambie ni nani aliyekugonga na tutakuamini." Hivyo sivyo. Ni kitu cha kumdhihirisha Mungu. Si kitu cha kumfanya Ndugu Weathers hapa, au Ndugu Shores, au Ndugu fulani nje huko, mtu mkuu, na kumfanya yeye mkuu kuliko watu wale wengine wa kundi lake, kumfanya yeye mtu aliye mkuu sana katika Phoenix. Si kumfanya William Branham kitu kikuu. Lakini inapaswa kufanya nini? Si kumfanya Oral Roberts kitu kikuu, Billy Graham kitu kikuu. Bali ni mioyo, tunajaribu kufikiliza jambo fulani kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Ni kumdhihirisha Mungu. Karama zote na kadhalika hazimfanyi mtu kuwa mkuu kuliko yule mwingine, zinatufanya sisi sote tu kufanya kazi pamoja kwa ajili ya ukamilifu wa ule mwili, kutuleta sisi pamoja kama watu wamoja, kama watu wa Mungu. Lakini uwaonapo wakienda kinyume, usiwalaani, waachilie tu, sharti mtu fulani afanye hivyo. Lakini ngoja hata Kristo atakapokuja katika nguvu.

56 Sasa tunawaona hao manabii wote wakinena. Kila mmoja wao alikuwa anamtukuza Mungu na Masihi ajaye. Na walipoingia katika Roho, wao walitenda na kunena na kuishi kama tu Masihi alivyofanya. Kama ilifanya hivyo upande huo wa msalaba, ikinena juu ya kuja Kwake, ni zaidi jinsi gani itakavyokuwa baada ya kuja Kwake, atakavyotia Roho wa Masihi Kanisani kutenda, kufanya, kufanya kazi, na kuishi kama Masihi? Ni Roho wa Mungu.

57 Pambanueni hiyo roho muone kama ni ya Mungu au la. Angalieni kama inatenda kama Yeye. Uone kama mwamusho wako. . .Kama mtu fulani anafanya jambo dhidi yako na kuyatupia uchafu maisha yako, nawe unajua huna hatia hata kidogo, na unajua ya kwamba una Roho wa Mungu, usijaribu kujitenga. Usijaribu kuwatendea vibaya. Usiwalaani. Endelea tu, ukijua ya kwamba Mungu alifanya hivyo kukupa wewe jaribio aone jinsi utakavyolichukua. Atalifikia kwa vyovyote.

58 Kama nilivyosema hivi majuzi, ninaamini katika kanisa la Ndugu Fuller, juu ya yule mwendeshaji baisikeli katika Canada. Vema, hao wote walidhani wangaliweza kumshinda kupanda baisikeli huyu maskini mvulana wa hali ya kike. Na alikuwa ndiye wa pekee ambaye hangaliweza kupanda bila kushikilia usukani.

59 Ninafuraha ninataka kuwa mmoja wa hao waendeshaji wakishikilia usukani wa kale, nishikilie pande zote za Msalaba na kusema, "Sina cha mkononi. Hebu niushikilie Msalaba, Bwana, sina ujuzi wa kiakili. Sina chochote. Hebu mimi nishikilie hapa tu, nitazame huko mbali sana."

60 Nao walikuwa na ubao upana wake inchi kumi na mbili kupandia baisikeli kwa umbali wa jengo moja la mjini, wapate baisikeli ya Schwinn ya dola mia moja. Wavulana wote ambao wangaliweza kupanda baisikeli bila kushikilia, waende mjini na kuwaletea mama zao vyakula na vifaa vya jikoni na kurudi bila hata kugusa usukani, kila mmoja wao alianza kutazama. Walikuwa hawajazoea kushikilia usukani, na ikaanguka. Lakini maskini mvulana huyu alifika pale na kushikilia usukani na akaiendesha hadi mwisho. Wakamuuliza, kasema, "Ulifauluje?"

61 Akasema, "Hapa ndipo mlikosea, wenzangu. Ninyi mnajua kuziendesha baisikeli vizuri kuliko mimi, bali mlikuwa mkitazama *hapa*," kisha akasema, "Iliwatia wasiwasi kuona kile. . . Mlikuwa mkijaribu kujiimarisha sawasawa, mkaanguka." Kasema, "Mimi sikutazama hapa hata kidogo, nilitazama kule mwisho nikaiendesha imara."

62 Hivyo ndivyo itupasavyo kufanya. Msiangalie mambo haya madogo sasa, "Huyu alifanya *hili* au yule alifanya *hilo*.?" Tazameni kule mwisho na mwe imara. Kristo yuaja. Tazameni kule mwisho, iweni tu imara. Msione kinachoendelea sasa. Tazameni kile kitakachotendeka huko ng'ambo wakati wa mwisho, ambako itatubidi kusimama na—na kutoa hesabu ya maisha yetu.

63 Daudi hakuwa akimtazama yule maskini Mbenyamini akimtupia uchafu, yeye alikuwa kiwete hata hivyo. Hakumuona yeye. Hata hangemruhusu mlinzi wake amkate kichwa, kasema, "Mwacheni, Mungu alimwambia afanye hivyo. Mungu alimwambia anilaani, mwacheni." Kwa maana Daudi alijua ya kwamba pana siku angalirudi katika mamlaka. Huyo Mbenyamini angekuwa na wakati wake.

64 Ndio, ndivyo ilivyo. Kanisa litainuka katika ushindi. Nilitumwa tu kuwaombea watoto Wake walio wagonjwa kwa vyovyote. Hayo ndiyo yote niwezayo kutenda. Popote walipo wala kanisa gani, si kitu kwangu. Ninajaribu kuwaombea watoto Wake walio wagonjwa, nikijaribu kuidhihirisha karama kwa ajili ya utukufu Wake. Hiyo ndiyo sababu sijapata kuwa mshirika wa kitu chochote.

65 Sasa, kumbukeni, hayo ni sawa. Mnaona, mimi si—mimi sisemi hilo sasa. Ninataka mnielewe wazi ya kwamba ninaamini Mungu ana Wakristo katika kila kanisa, watoto Wake, Yeye hajaniuliza kamwe juu ya hilo. Nilitumwa tu kuwaombea watoto, na kufanya mambo haya, na kumdhihirisha Yeye.

66 Sasa, mnaona, Yesu na hawa manabii, kila kitu walichonena juu yake, kilibidi kuwa kweli, kwa sababu zilikuwa ni nguvu za Mungu ndani yao, Mungu Mwenyewe akinena kupitia kwao juu ya Nafsi Yake akija utukufuni Mwake.

67 "Rais ni nani? Ni nani atakayekuwa, atakayekuwa? Tutapata mvua ya kutosha mwaka huu?" Hiyo haimaanishi chochote. Kitu fulani kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kitu cha kuliweka Kanisa katika utaratibu, kitu fulani kwa ajili ya nguvu za Mungu; si kujifanyia jina, bali kuufanya utukufu wa Mungu udhihirike.

68 Sasa tunaona ya kwamba manabii hao wote na yote waliyosema humhusu Yeye, kila kitu kilitimilika kwa sababu Yeye alikuwa kiini cha Agano la Kale. Yesu, yule Masihi, Masihi ajaye, ndicho kitu ambacho nabii alitazamia toka—toka Adamu hadi Malaki. Kila nabii alinena, juu ya kuja kwa Bwana. Kila mmoja alitia sehemu yake kwa sababu alitiwa upako wa Mungu. Hayo ndiyo yote angaliweza kunena juu yake.

69 Sasa, ningependa kama tungekuwa na muda zaidi juu yake. Lakini, chunguza, kila kitu ambacho wao walisema kilitimia. Tazameni hapa, hebu na tuchukue tu baadhi ya mambo waliyosema manabii.

70 "Bikira atachukua mimba na kuzaa mwana." Je, ilitukia? Bila shaka. "Jina Lake ataitwa Imanueli, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Enzi, Baba wa milele." Hivyo ndivyo alivyokuwa, hasa, "Baba wa milele." Hakuna mtu atakayeitwa "Baba," humu duniani, bali Mungu ni Baba yenu.

71 Sawa, sasa hebu na tuone tena. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, kwa mapigo Yake tuliponywa." Chumbani cha hukumu cha Pilato, wakati mtu yule yule, baada ya kumfanya apigwe sana mgongoni mwake na mjeledi wenye ncha tisa zenye mafundo, hakutambua ya kwamba Maandiko yalisema ingalikuwa hivyo. Hawakuwa na upambanuzi wa roho, hao makuhani waliosema "Mwondoshe, mwondoshe."

72 Na akiwa msalabani walipomfyonyezea midomo yao, na mambo kama hayo, walipomsikia Yeye akilia, "Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Hawakuwa na upambanuzi. Mnaona, hawangaliweza kupambanua Roho. Hayo ndiyo Daudi aliyokuwa akiyanena katika Zaburi ya 22, walifyonya midomo yao bila kujua walikuwa wakifanya hivyo. Sawa tu na yule Mbenyamini alivyomfanyia Daudi. Mwaona, alifikiri Daudi alikuwa amekosea kabisa kwa sababu hakukubaliana naye katika kanuni zake za kuendesha ufalme wake. Hakufahamu

ya kwamba ilikuwa ni Roho wa Mungu akifanya hivyo katika Daudi.

73 Hapo ndipo ni lazima tupambanue, leo, roho ya mtu. Ni nini anajaribu kufanya? Analenga nini? Sio kikundi anachohusika nacho, au nini *hili*, *lile*, au *lile lingine*, kwamba ni mtu mweupe, mtu mweusi, mtu manjano, au chochote kile. Hebu na tuone ni nini anachojaribu kufikiliza, na kutwaa hicho, tuone kile anachojaribu kufanya kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Ana mawazo tofauti na yetu, hilo ni sawa hasa iwapo anajaribu kufikiliza kitu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Pambanua hilo ndani yake. Iwapo amekosea, na ni mweupe moyoni mwake, Mungu atamleta hata kwenye Ukweli wa lile jambo baada ya kitambo kidogo. Mwachilie, mwachilie, uone kile anachojaribu kufanya.

74 Sasa tunaona hapa, kisha tunagundua katika ki—katika kifo Chake, alipokufa msalabani, na kupaza sauti juu ya mambo yote waliyonena manabii juu Yake; "Wamenizua mikono Yangu na miguu Yangu." Hapo ilitimizwa. Manabii walikuwa sahihi. Walidhani walikuwa ni wao wenyewe au walipaza sauti kama kwamba ni wao wenyewe, bali ilidhihirishwa msalabani.

75 "Yeye—Yeye alihesabiwa pamoja na hao wakosao." Hivyo ndivyo alivyofanyiwa. Yeye alikuwa pamoja na hao wakosao. "Katika mauti Yake Yeye alizikwa pamoja na matajiri." Alifanya hivyo, Yeye alizikwa katika kaburi la tajiri. "Sitaiacha nafsi Yake . . . Hatakuachia kuzimu nafsi yangu," Daudi alisema, Roho wa Mungu akisema katika Daudi. "Hutakuachia kuzimu nafsi yangu, wala hatamwacha Mtakatifu Wake auone uharibifu," kama kwamba Daudi angalikuwa Yule mtakatifu. Haikuwa Daudi, ilikuwa ni Roho wa Mungu akipasa sauti ndani ya Daudi. Mnaona, Roho wa Mungu akipasa sauti ndani ya yule mtu.

Mtu fulani alisema, "Msimsikize maskini mnafiki yule kule."

76 Haikuwa yeye, ilikuwa Roho wa Mungu akipasa sauti ndani yake. Mnaona, Roho wa Mungu hujionyesha mwenyewe, "Hatakuachia kuzimu nafsi Yake, wala hatamuacha Mtakatifu wangu auone uharibifu."

77 Sasa, ndugu zanguni, nikimalizia, hebu niseme hili, wakati wetu umemalizika. Lakini, angalieni, hebu niseme hili nikimaliza, pamoja na Maandiko haya hapa. Hebu tuone. Kama mtu, ambaye kiini chote cha Agano la Kale kilikuwa juu Yake, manabii wote watakatifu waliokuwa na upako wa Roho wa Mungu, kama hayo yote na kila kitu walichonena kilitimilizwa kabisa katika Yeye, hakika huyo mkuu aitwaye Mwana wa Mungu yampasa kujua jinsi ya kulianzisha Kanisa la Agano Jipya. Si mnaamini hivyo? Yampasa Yeye kuwa na wazo la kujua jinsi ya kuliunda Kanisa la Agano Jipya.

78 Jambo la kwanza ninalotaka kuwakumbusheni, hapa katika Mathayo, sura ya 16, kwamba Yeye—Yeye alipokuwa akinena wakati huo, aliposhuka chini na akawa akiwazungumzia mitume. Yeye alisema, “Watu hunena kuwa Mimi Mwana wa Adamu ni nani?”

79 Nao wakasema, “Wengine hunena Wewe ni ‘Eliya,’ na wengine hunena Wewe ni ‘Fulani,’ na wengine Wewe ni ‘Fulani,’ na vivyo hivyo, watu mbalimbali.”

Alisema, “Bali *ninyi* mnasema Mimi ni nani?”

80 Kisha Petro akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

81 Yeye akasema, “Heri wewe Simoni, Bar-Yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia wewe hili. Nami—nami nakuambia, wewe ndiwe Simoni, au Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda.” Sasa pale alikuwa akinena kuhusu Kanisa. Sasa angalieni kwa makini, na iwapo nimekosea, Mungu anisamehe nanyi mnisamehe.

82 Sasa, ka—kanisa Katoliki husema kuwa “Hilo lilikuwa jiwe pale, *Petro,* na juu ya Petro Yeye alijenga Kanisa.” Sasa tunajua kuwa hilo ni kosa. Sisi Waprotestanti hatukubaliani nalo.

83 Lakini sisi Waprotestanti tulisema, “Ni juu Yake *Mwenyewe* alikojenga Kanisa Lake, Mwenyewe.” Bali, kama utatambua, nataka kutokubaliana na hayo, kirafiki. Haikuwa hivyo.

84 Ilikuwa juu ya *ufunuo* wake Mwenyewe wa kiroho. Mnaona? “Mwili na damu. . .Hukusoma hili kamwe katika seminari, zikiwa nzuri kama zilivyo. Hukusoma hili kwa baadhi ya kanuni ya imani ya kanisa, ikiwa nzuri kama ilivyo. Ni sawa, bali mwili na damu havikukufunulia hili. Sio wazo la kiakili la jinsi unavyoweza kufanya usemi wako, jinsi inavyokulazimu kujiinamisha, jinsi au ni jambo kuu lipi linalokulazimu kutenda hapa duniani. Hivyo sivyo lilivyo. Sio kujenga kitu kikuu wala kufanya jambo kuu. Jambo hilo ni ufunuo wa Neno la Mungu. Yeye alikuwa Neno. “Hapo mwanzo kulikuweko Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akadhihirishwa akakaa kwetu.” Yeye alikuwa . . . huo ulikuwa ufunuo wa Neno la Mungu.

85 Roho ndani ya Petro akifunua kwa ufunuo wa kiroho ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu akidhihirishwa. Mungu wa Utukufu akionyesha utukufu wa Mungu. “Juu ya mwamba huu (ufunuo wa kiroho wa Neno) nitalijenga Kanisa Langu.” Kwa nini? Kama hao manabii walikuwa chini ya Mungu, wakinena kwa Roho Mtakatifu ya kwamba huyo alikuwa Mwana wa Mungu, Roho yuyo huyo upande huu anafunua jambo lile lile tena. Mnaliona?

86 "Mwili na damu," huwezi kulisoma katika seminari. Unapojifunza ninino. . .unapata D.D. yako na Ph.D yako na L.D., au. . .Hizo ni sawa, laiti ningalikuwa nayo. Hiyo ni kweli, bali hata hivyo hiyo siyo. Si lazima uwe nayo, ingawa ni vizuri kuwa nayo. Unaweza kuwa Hili, na zaidi; bali ikikulazimu kuondoa iliyo zaidi, twaa Hili. *Hili* ndilo Lile. Kama hili silo Lile, hebu niwe na Hili kwa vyo vyote. Nataka Hili! Hili!

87 "Mwili na damu havikukufunulia hili." Hukujifunza kamwe hili kwa njia ya elimu. Hukujifunza hili kamwe kwa njia za kidhehebu. Ni nzuri, elimu, dhehebu ni nzuri. Hiyo ni sehemu yake. Lakini watu wanategemea hayo sana na kuachilia mbali upambanuzi wa kiroho. Mnaona?

88 "Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda." "Haitaweza kamwe kulishinda," ilionyesha ingalikuwa ikishindana Nalo.

89 Sasa chungulia na uone ni wapi milango ya kuzimu inaposhindana. Haishindani na madhehebu. Serikali hutambua hayo. Sivyo. Ulimwengu unatambua madhehebu yetu, yote. Tuna haki, kila mmoja wetu kama raia wa Marekani, tuna haki za dhehebu, ambayo ni sawa, tunashukuru kwa ajili yake. Bali hiyo siyo milango ya kuzimu inashindana nayo. Inashindana na ufunuo wa kiroho wa Kristo akiwa hapa sasa, yeye yule jana, leo, na hata milele. Hicho ndicho inashindana nacho. "Milango ya kuzimu itashindana nalo, lakini haitalishinda."

90 Ndivyo hivyo, upambanuzi wa kiroho. Bila kujali ni nani, ni ndugu yangu mradi tu yeye anajaribu kufikiliza kusudi lile lile ninalojaribu. Hebu awe ni nabii, hebu awe mchungaji, hebu awe shemasi, hebu awe fulani, hebu na Mungu amheshimu kwa njia *hii*, na kwa njia *ile*, chochote kile, asiniheshimu, chochote anachotaka kutenda, lakini bado huyo ni ndugu yangu. Tunafanyia kazi jambo lilo hilo. Tunatuma ka—kazi zetu zote katika Ufalme ule ule huko ng'ambo. Anafanyia kazi jambo lile lile ninalofanyia. Upambanuzi wa kiroho, ufunuo wa kiroho wa Mungu. Tazama hapa, kama ukitaka.

91 Yesu. . .Nilihubiri hivi majuzi usiku mahali fulani, labda kule chini, "Tangu Mwanzo Haikuwa Hivi." Yatubidi turudi nyuma mwanzoni kutafuta fungu letu sasa kwa muda mchache. Hapo mwanzo alikuweko Kaini, mwenye akili, alijenga kanisa nzuri (tungesema), alitengeneza madhabahu mazuri, alitoa dhabihu, aliomba, kwa moyo mnyofu, alitoa shukurani, alilipa zaka zake, kila kitu akiwa wa kidini kama tu Habili alivyokuwa.

92 Lakini Habili, (hawakuwa na Biblia siku hizo,) bali kwa ufunuo na Kiroho aliona ya kwamba haikuwa matunda ya bustanini yaliyotufanya tutende dhambi, sio matofaa waliyokula. Mnaona, hayakuwa matofaa, ufunuo ulimwambia

hivyo. Na hayakuwa matunda yaliyomfanya aondoke pale. Ilikuwa uhai, utenganisho wa uhai; kwa hivyo alienda na kumpata mwana-kondoo na kumtoa sadaka mahali pake kwa imani, ambayo ni ufunuo wa kiroho. Amina! Ufunuo wa Mungu, ufunuo wa kiroho ambao ulifunuliwa kwake. Si tunda, sio matofaa, sio maembe, zambarau na mapera. Ilikuwa utenganisho wa uhai, kwa hivyo alienda akautwaa uhai na kuutoa sadaka badala ya matunda.

93 Matunda ndiyo unayokula, kazi zako mikononi mwako. Kile ufanyacho pale, "Nitaenda na kujenga *hili*. Nitaenda na kufanya *hili*. Nitaunga mkono *hilo*." Sawa. Alikuwa na madhabahu sawa sawa tu na vile alivyokuwa yule mwingine. Wote wawili walikuwa na madhabahu. Hiyo ilikuwa nzuri.

94 Lakini ulikuwa ukweli uliofunuliwa kiroho wa jambo hilo, kwa kuwa Roho wa Mungu aliufunua, "Na juu ya mwamba huo, mwamba ambao Kristo alikufa juu yake, Mwamba wenye Imara, mwamba ambao juu yake mwana-kondoo wa Habili alikufa." Huyo kijana Habili mdogo alipokuwa akiweka mikono yake juu ya Huyo mwana-kondoo mdogo, na yale manyoya yake madogo meupe yakilowa alipoutwaa mwa—mwamba, hawakuwa na kisu siku hizo, na kumkata shingo yake dogo namna hiyo na kumtwanga. Na maskini kitu kidogo kikifa, damu ikiilowesha mikono yake, na manyoya yake madogo yakilowa damu, akipiga makelele na kulia.

95 Ilinena juu ya nini? Mwana-Kondoo wa Mungu miaka kama elfu nne baadaye, ilionyesha kiroho kanisa likimkataa Yeye. Na watu walimwita Yeye "Belizebuli" na "pepo," kwa maana manabii wote walikuwa waishasema. Wao hukataa nabii. Lo, Yeye alisema, "Mnajenga makaburi yao, na mliwatia huko. Enyi kuta zilizopakwa chokaa," Yeye aliwaambia. Bila upambanuzi wa kiroho, bila kujua kwamba huyo alikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu. Ya kwamba ilimpasa kuwa hivyo na kutenda hivyo, maana alikuwa akilitimiza Neno la Mungu.

96 Na Kanisa la Roho Mtakatifu siku hizi, wakitenda jinsi wanavyotenda, wakifanya mambo wanayofanya, wao wanatimiza Neno la Mungu. Haleluya! Mnaona, Petro alisema, siku ya Pentekoste, "Hili ni lile". Naye alisema, "Ni kwa ajili yenu na watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Mungu wetu wamjie."

97 Hao manabii waliokuwa na uvuvio walisema Nuru ya jioni ingaling'aa, kungekuwa na mvua ya masika na mvua ya vuli pamoja kama katika siku za neema. Tazameni hapa. . .Ni nini? Mvua za masika zikija, huku mvua ya vuli wakati wake umekwisha pita. Basi ni kupitana, na ziko pamoja, mvua ya masika na ya vuli pamoja, Roho Mtakatifu akidhihirishwa kwa nguvu na ufufuo wa Yesu Kristo. Ndivyo hivyo, zikija pamoja, ya masika. . .Neema ya Mungu! Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa

katika siku za Nuhu." Neema Yake ilikuwa ikivumilia. Na ndiyo hii hapa leo, uvumilivu, kupitana. Inaleta wingu toka siku za kale na wingu kutoka siku hizi, pamoja. Mvua ya masika huja kwanza, mvua ya kwanza tumekuwa nayo, sasa hapa yaja mvua ya vuli, mvua ya masika inakuja juu ya mvua ya vuli, mashariki na magharibi zikikutana. Mvua zote mbili zikija pamoja, uponyaji wa Kiungu pamoja na Malaika wa Mungu akifunua siri za mioyo na kufanya kila kitu kitimie. Lo, yaonekana kama watoto halisi wa Mungu wangeona hilo. Ndivyo hivyo, Roho akifunua ufunuo. Huo ndio ule Yesu alisema Kanisa lingejengwa juu yake.

98 Vema, basi mtu fulani angaliweza kuinuka na kusema, "Vema, hakika, sisi Fulani na fulani, tulijengwa juu ya Huo."

99 Hebu na tulichukue Neno Lake hatua nyingine. Lile agizo la mwisho kwa Kanisa Lake, Yeye alisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Ulimwenguni kote. Itaendelea mpaka wapi? Ulimwenguni kote. Kwa wangapi? Kila kiumbe. "Yeye aaminiye na kubatizwa," sio kanisa, "yeye" ni kijina. "Yeye aaminiye," mtu binafsi.

100 Kama David DuPlessis alivyosema juu ya wajukuu hakuna wajukuu katika Ufalme wa Mungu ni watoto! Babako alikuwa Mpentekoste nawe unakuja tu katika kanisa hili kwa sababu yeye alikuja hapa kwenye—kwenye Eleventh na Garfield, akampokea Roho Mtakatifu, naye alikuleta humu tu kama mjukuu, umekosea! Inampasa Mungu ajifunue Yeye Mwenyewe kwako.

101 Na hakuna mtu anaweza kumwita Yesu Kristo kwa wazo la kiakili. Hakuna mtu anaweza kumwita Yesu Kristo kwa sababu anasikitikia dhambi zake na anakuja kutubu. Hakuna mtu awezaye kumwita Yesu yule Kristo, ila tu kwa. . .huo ufunuo wa Roho Mtakatifu, ukimfanya ajulikane naye. "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayatalishinda." Huo ndio ufunuo. Ndio huo, alikolijenga Kanisa Lake.

102 Ni nani aliyefanya hivyo, Petro? La, la, la. Ni nani aliyefanya hivyo? Kristo alisema, "Ufunuo wa Mungu, Roho Mtakatifu atauleta kwako. Kitambo kidogo na nitawaacheni, bali nitamuomba Baba naye atawapelekeeni Msaidizi, atakayewakumbusha mambo haya." Hiyo ni kweli? Kile Yeye anachofanya asubuhi hii. Na atafanya nini? "Kuwaonyesheni mambo yajayo." Roho Mtakatifu Kanisani katika siku za mwisho.

Sasa mnasema, "Ndugu, haleluya, hilo ni kanisa langu."

103 Ngoja kidogo! Yesu alisema, "Hivyo watu watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu," katika Yohana Mt. 13:35, "Hivyo watu watatambua ya kuwa ninyi ni wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Ukweli wa Ufalme

ujao wa Mungu, uliofunuliwa na Roho, ukitazamia huko mwisho, ukiangalia kile manabii walichopasia sauti, ukiona kile Yesu alichonena juu yake, na hapa Roho Mtakatifu yule yule ndani yako anaitikia papo hapo, "Hiyo ni kweli! Hiyo ni kweli!" Ni nini? Ni Ukweli uliofunuliwa kiroho. Nawapenda ndugu zangu bila kujali kanisa waendalo, hata wawe ni wa mvua ya masika au vuli, au si wa mvua iwayo yote, mradi tu wamo katika Mwili wa Kristo, wakijaribu kufikiliza. Si kitu fulani kwa ajili ya kusudi fulani ku—kujionyesha mwenyewe nchini, bali kwa kusudi la Ufalme wa Mungu na utukufu wa Kuja Kwake, kufunua na kutujulisha kule Kuonekana Kwake hivi karibuni.

104 Sasa, katika kumaliza, tunataka kuwazia hili. "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu," sawa. Na ndiposa tunaona, pale katika Yohana 14:7, Yeye alisema hivi, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Kazi nizifanyazo Mimi." Ni kazi za namna gani alizozifanya kujifanya Mwenyewe ajulikane? Mnakumbuka juu ya Petro, sivyo? Kile tulichokuwa tukinena juu yake, Filipo, yule mwanamke kisimani. Akitabiri isiwaendee Mataifa, ila ingalikuwa katika siku za mwisho, kama alivyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika siku Zake Mwana wa Adamu." Kuna ufunuo ulioandikwa katika siri kama hii, kwa ulimwengu wa nje, kwa ulimwengu usiojua chochote juu yake. Bali ninyi ndugu wa thamani, ninyi dada wa thamani, ninyi si wana wa giza, ninyi si wana wa usiku, bali ninyi ni wana wa Nuru. Mkienenda Nuruni kama Yeye alivyo katika Nuru, basi mwashirikiana ninyi kwa ninyi, huku Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yatusafisha dhambi zetu zote kutoka kwetu sote. Ndivyo hivyo, watumishi wa Bwana.

105 Yesu. . .Ninaponukuu Andiko langu hapa, nina Marko 16, ndio Marko 16, ilisema, "Enendeni ulimwenguni mwote." Hii ndiyo namna ya Kanisa aliloanzisha. Agizo la mwisho kwa Kanisa, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa." Sasa tazama hapa, tazama huku kupambanua kwa kiroho. . . "Aaminiye na kubatizwa." Yeye hakusema kamwe hasa kwa njia gani, lakini tunataka kubishana juu ya hilo, mnaona, jambo lingine. Mnaona, "Aaminiye na kubatizwa ataokoka." Jinsi anavyotaka kubatizwa, hilo ni juu yake. Ikiwa kitendo chake ni kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, endelea, ndugu. Tunapiga hatua kwa Roho yule yule. Kama nimekosea, basi utajua, itatokea kwa njia hiyo. Na kama umekosea, itakuwa hivyo. Lakini mioyo yetu na nia zetu na shabaha zetu ni kwa ajili ya Ufalme wa Mungu kule ng'ambo. Tuko ng'ambo, twaelekea Kalvari.

106 Mimi na nia zangu, kwani, nina. . .Sina ndugu apendaye sambusa ya matunda kama zambarau vile nipendavyo, bali sisi ni ndugu. Mwaona? Hakuna mmoja wao apendaye kuwinda na

kuvua samaki kama nipendavyo, bali sisi ni ndugu. Mnaona ninalomaanisha? Nina mawazo yangu, bali hiyo haimfanyi kutokuwa ndugu yangu, babaye ni babangu, jamaa yake ni jamaa yangu. Ndivyo hivyo.

107 Wale wazee wetu wote walitofautiana wao kwa wao, lakini kulikuwako na baba mmoja, na yapaswa itende kazi kuwa kitu kimoja, nao walimkataa aliyekuwa mkuu mle kwa sababu alikuwa wa kiroho. Hamlioni ndugu zanguni? Hamwezi kukiona kile ninachozungumza juu yake?

108 Sasa angalieni katika . . . hebu mimi . . . kumalizia, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka. Yeye . . . " [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya." Ni nini? Ufunuo wa kiroho. Mnaona? "Watasema kwa lugha mpya. Wakishika nyoka ama wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Hivyo ndivyo lilivyokuwa lile Kanisa Jipya. Hiyo ndiyo aina ya Kanisa ambalo Yesu Kristo, huyo Mkuu Mmoja, ambaye manabii wote walipasa sauti kwamba angetenda. Tunaona Roho Wake huja hapa na kutabiri ya kwamba Roho Wake katika watu angerudi na kutenda mambo ambayo Yeye aliyatenda.

109 Hebuni nimalize kwa kusema hili. Ninayo Maandiko kama dazani moja au zaidi hapa, lakini hatuna wakati. Mwaona? Bali sikilizeni hili. Hebuni nimalizie kwa kusema hili. Kila nabii wa Bwana aliyezaliwa mara ya pili kweli kweli, mhubiri, mwalimu wa shule ya Jumapili, mwonaji, mtume, mmishenari, ye yote yule, moyo wake wote umeandaliwa, naye amejawa na kuwa na upako sana wa Roho wa Mungu, ana upako sana. Hata kazi yake iwe nini, chochote kile, kuhubiri, au kufundisha, au kufanya uinjilisti, au kuona maono, chochote kile, atafanya kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Naye Roho wa Mungu atanena papo hapo kupitia kwa huyo mtu na kudhihirisha ni Ufalme wa Mungu.

110 Ndiposa sisi . . . Mimi kama Mbatisti, ninawaona ninyi Wapentekoste, ninyi ni ndugu zangu. Ninyi si wa kanisa la Kibatisti, mimi nilikuwa walo. Hilo ndilo kanisa pekee nililowahi kuwa mshirika wake, lilikuwa kanisa la Kibatisti. Lakini hilo halinizuii, ninaona ni Roho gani wa Mungu aliye pamoja nanyi. Ninaona kile mnachojaribu kufanya. Vema, ikiwa mimi, Mbatisti, naweza kujisikia hivyo, bila shaka wa Assemblies, Church of God, Muungano wa Wapentekoste, Independents, na sisi sote ndugu pamoja yatupasa tuone ya kwamba tunajaribu kufanya kazi kwa kusudi moja. Hebu tuwe na upambanuzi wa kiroho.

111 Sasa sikilizeni. Katika kumaliza, nitataja neno hili la mwisho. Wengi ni wagonjwa na wadhaifu miongoni mwenu,

na wengi wamelala, wamekufa kiroho, kwa sababu hawana upambanuzi wa ule Mwili wa Kristo. Huu mwili mgonjwa tulio nao! Mungu atusaidie tuwe na upambanuzi wa kiroho wa huo ufunuo wa Ufalme wa Mungu na wa upendo wa Mungu mioyoni mwetu, ukinyunyiziwa kote na Roho Mtakatifu, tujaribu kuinyosha mikono yetu mbali sana, tuseme, "Sisi ni ndugu." Mnaona ninachomaanisha? Na kila karama dogo mliyo nayo, msiitumie kujaribu kuifanya kitu fulani kikuu kwa ajili yetu wenyewe, hebu tuifanye kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, tukifanya kazi na kila mtu, tukijaribu kuinua kusudi la Yesu Kristo, kwa sababu Kuja Kwake ku karibu. Je, mnaliamini?

112 Nasikitika kwa kuwakawisha muda mrefu hivi. Ndugu David atakuwa hapa kesho kuwafundisheni Maandiko, lakini hivi sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa kitambo tu. [Ndugu yuanena kwa lugha nyingine. Dada yuatoa tafsiri—Mh.]

Twendeni askari!
Watu wa Mungu;
Yesu yuko mbele,
Tumwandame juu;
Ametangulia Bwana vitani,
Twende mbele kwani ndiye amini.

Twendeni askari! (unaamini ndivyo ulivyo? inua mkono wako)
Watu wa Mungu, (tukiwa na nini?)
Yesu . . . (lengo letu) yuko mbele,
Tumwandame juu.

Mungu awabariki. Mchungaji wenu.

*Upambanuzi Wa Roho* SWA60-0308
(Discernment Of Spirit)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne asubuhi, Marchi 8, 1960, katika First Assembly of God kule Phoenix, Arizona, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1989 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org